

Kamati za Bunge kuanza kesho bila nyenzo

Wakati Kamati za Bunge zikianza kesho (Jumatatu) ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya Kikao cha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012, bado Wabunge hawajakabidhiwa vitabu vya makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka huo wa fedha hali ambayo itadhoofisha uwezo wao wa kuchangia mjadala wake ipasavyo.

Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mh. Zitto Kabwe, ameithibitishia Sikika kwamba hadi sasa vitabu hivyo havijapatikana na haijulikani vitapatikana lini, “Ni kweli kwa mujibu wa mabadiliko ya kanuni za Bunge ya mwaka 2007, tunatakiwa kupewa vitabu hivyo siku 21 kabla ya kikao cha bunge kuanza lakini kusema kweli haijawahi kutokea,” anasema Mh. Kabwe ambaye amekuwa mbunge kwa miaka sita sasa. “Kwa kweli hili ni suala linalotakiwa kuhojiwa, na tutahoji.”

Naye Bi. Maida Hamada Abdalah (Wete), amesema kuwa ingawa hajapata kitabu hicho anaamini kuwa kwa vile vikao vya Kamati za Bunge zinaanza kesho (Jumatatu) atapata nakala yake wakati huo. “Kamati hizo zitaendelea kwa wiki mbili, na endapo havitapatikana hadi wakati huo ndio tutakuwa na maswali,” anasema. Katibu wa Ofisi ya Bunge, Bw. Emmanuel Mpanda, alipohojiwa sababu ya kutopatikana kwa vitabu hivyo kwa mujibu wa kanuni alionekana kushangaa kama kuna kanuni ya aina hiyo na kuhoji ni kanuni namba ngapi. Alipoambiwa na kusomewa kanuni hiyo akahoji, “Sasa ninyi ndio mmekuwa wasemaji wao, ninyi vitabu vya kazi gani na si kwa ajili yenu?”

Kwa kujua wabunge ni wawakilishi wa wananchi, Sikika ilisema kuwa kama wadau ilikuwa ikifuatilia kuona kama wawakilishi wao wana nyenzo za kufanyia kazi ambapo Bw. Mpanda aliingilia na kusema, “Kwa taarifa yenu vitabu hivyo si vya wadau na Kamati hizo si *public hearing* (za kuhudhuriwa na wananchi).


Kwa mujibu wa Ibara ya 96 ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la mwaka 2007), “Waziri (wa Fedha) atapeleka kwa Katibu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Serikali ya Mwaka wa Fedha unaohusika na nakala ya Makadirio hayo itapelekwa na kumfikia kila Mbunge angalau siku 21 kabla ya Mkutano ambao utashughulikia makadirio hayo.”

Wakati Bunge la Bajeti litaanza Juni, 7, 2011, hadi sasa ikiwa ni siku 16 kikao hicho kianze, wabunge hawajapata nyaraka hizo muhimu na Sikika imebaini kwamba imekuwa ni kawaida kwa Wabunge kupokea vitabu vya bajeti kwa kuchelewa sana, na wakati mwingine hupokea wakati kikao cha bajeti tayari kimeshaanza. Kuchapishwa kwa bajeti ya taifa kwa wabunge na umma kwa ujumla, ni hatua muhimu katika kuongeza uwazi, ubora na ufanisi katika bajeti.

Kutokana na hali hiyo, Sikika inajiuliza kwa hali hiyo kama kweli wabunge hujua bajeti wanayokuwa wakipitisha wakati wa kikao. Bajeti ya nchi si mchezo na huwasilisha takwimu nyingi hivyo wabunge wanahitaji muda mwingi zaidi kusoma taarifa hizo na kuzichanganua kuona manufaa yake kwa wananchi ili kuweza kufanya maamuzi sahihi.

Sikika inaamini kuwa kitendo cha wabunge cha kuidhinisha katika miaka ya hivi karibuni sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba mbili za makazi ya Magavana wa Benki Kuu (BOT) na sh. Bilioni 3.7 nyingine kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya makazi ya Spika huko Dodoma hatua ambazo zimelalamikiwa na wananchi na wabunge wenyewe wakiwemo ni matokeo ya wabunge kutopewa taarifa sahihi mapema na hatimaye kuwatwisha watanzania mzigo wa kulipia gharama hizo huku maisha yao yakizidi kuwa duni.

Ili kuwawezesha wabunge wetu kuchangia vizuri maendeleo ya wananchi na hatimaye ya taifa letu kwa ujumla, Sikika inaitaka serikali kuwapatia haraka Wabunge nyaraka muhimu kama vile vitabu vya bajeti ili waweze kupata muda wa kutosha kuchambua na hatimaye kuchangia mjadala wa hotuba ya bajeti ambayo ni uti wa mgongo wa matumizi ya mapato ya serikali.



Mr. Irenei Kiria

Mukurugenzi wa Sikika, P.O.Box 12183 Dar es Salaam,

Simu: +255 222 666355/57, Nukushi: 2668015, Barua pepe: info@sikika.or.tz, Tuvoti: www.sikika.or.tz

